

Ufungamano wa tamathali za semi na maudhui : Uchunguzi wa nyimbo za Unyago wa mwanahiti wa Wazaramo

Tunu Mayemba

M.A. (Kiswahili)

Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Institute of Kiswahili, 2016

Utafiti huu unaohusu ufungamano wa Tamathali za Semi na Maudhui: uchunguzi wa nyimbo za unyago wa mwanahiti wa Wazaramo ulisukuma na ukweli kuwa suala la ufungamano wa fani na maudhui katika nyimbo za unyago, halijashughulikiwa vya kutosha. Hivyo, utafiti huu ulikusudia kueleza unyago wa Wazaramo na nafasi ya nyimbo za unyago wa Mwanahiti wa Wazaramo na; kujadili ufungamano wa tamathali za semi zilizojitokeza na maudhui. Ili kutimiza malengo hayo, utafiti huu ambao data yake ilikusanywa katika mkoa wa Pwani na Dar es salaam ulitumia mbinu ya mahojiano, ushiriki, ukusanyaji matini na utafiti wa maktabani. Pia, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya usosholoji na nadharia ya umuundo na mkabala wa kitaamuli katika kuchambua na kutafsiri data zilizokusanywa. Matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba unyago katika jamii ya Wazaramo, ni asasi muhimu snaya kurithisha amali mbalimabli. Pia, imebainika kuwa kuna aina mbalimabali za unyago katika jamii ya Wazaramo ambazo zinatumia nyimbo zilizosheheni tamathali za semi. Si hivyo tu bali pia imebainika kuwa kuna ufungamano mkubwa baina ya tamathali za semi zilizotumika na maudhui yanayowasilishwa na nyimbo za unyago wa Mwanahiti. Tamathali mbalimali za semi zinanaonekana kuisaidia kuibua dhamira, kutambulisha wahusika, kubeba falsafa na dhima nyingine kadhaa wa kadha za kifani na kimaudhui. Ingawa utafiti huu umejadili kwa kina masuala mbalimabli yanayohusiana na ufungamano wa fani na maudhui katika unyago wa Wazaramo, bado panahitajika utafiti za kina kushughulikia ufungamano huo katiak tanzu nyinginezo za fasihi ili kuweza kutoa mahitimishi jumuishi. Pia, kwa utafiti huu ulihusu aina moja ya unyago wa Wazaramo, unyago wa Mwanahiti, kuna haja ya kufanya utafiti katiak aina nyingine za unyago wa jamii hii na hata jamii nyinginezo. Aidha, kuna haja ya kufanya utafiti wa ufungamano wa vipengele vingine vya fani katika kuwasilisha ma